BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA SHERIA, UTAWALA BORA NA IDARA MAALUM JUU YA UWASILISHWAJI WA RIPOTI YA MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR KWA MWAKA 2018

Mheshimiwa Spika; awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Muumba wa mbingu na ardhi, kwa kutujaalia afya njema na taufiki na kutuwezesha kukutana hapa leo hii kwa ajili ya kuendeleza majukumu yetu muhimu ya kuishauri Serikali pamoja na kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar katika chombo hiki muhimu ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika; aidha, natumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili kutoa maoni ya Kamati yetu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum juu ya uwasilishwaji wa Ripoti ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar kwa mwaka *2018*.

Mheshimiwa Spika; vilevile, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu, Ripoti ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar. Ripoti hii inaonesha utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka kama Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar, nambari *1* ya mwaka *2012*, inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika; kwa dhati kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii ya Sheria, Utawala Bora na Idara

Maalum kwa mashirikiano yao makubwa yanayoendelea katika Kamati hii kwa kuonesha ufanisi mkubwa katika kutimiza wajibu wao katika chombo hiki kitukufu katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naomba niwataje Wajumbe wa Kamati hii ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kama ifuatavyo:

1. Mhe. Machano Othman Said - Mwenyekiti
2. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Khamis Bakar - Mjumbe
4. Mhe. Ramadhan Hamza Chande - Mjumbe
5. Mhe. Suleiman Makame Ali - Mjumbe
6. Mhe: Maryam Thani Juma - Mjumbe
7. Mhe. Salma Mussa Bilal - Mjumbe
8. Ndugu Haji Jecha Salim - Katibu
9. Ndugu Ali Alawy Ali - Katibu

Mheshimiwa Spika; aidha, nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati viongozi na watendaji wote wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Unguja na Pemba kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao bila ya kujali ugumu wa kazi wanazozifanya katika kusimamia haki na wajibu wa wananchi katika kulinda na kusimamia uchumi wa Zanzibar, licha ya changamoto mbalimbali zinazojitokeza na kukabiliana nazo ikizingatiwa kwamba suala la kukabiliana na vitendo vya rushwa ni gumu na linaleta kila aina ya changamoto kwa wahusika wanaopinga vitendo hivi.

Mheshimiwa Spika; Kamati yangu inapongeza kwa dhati mashirikiano yaliopo baina ya Mamlaka hii na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM), Jeshi la Polisi, DPP pamoja na raia wema. Hata hivyo, Kamati inaiomba Mamlaka hii kuzidisha mashirikiano na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ili waweze kubadilisha uzoefu utakaoboresha utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika; vilevile, Kamati inaishauri Mamlaka kuhakikisha kuwa inazidisha juhudi zao za kutoa uelewa kwa wananchi juu ya madhara ya rushwa na uhujumu wa uchumi kwani kiuhalisia bado vitendo hivyo vinaendelea kufanyika katika jamii yetu kwa mujibu wa Takwimu zilizotolewa na Mamlaka, tuhuma za makosa ya rushwa zimeongezeka kutoka *187* hadi *209* kwa mwaka *2018*.

Mheshimiwa Spika; aidha, Kamati yetu inatoa pongezi kwa Mamlaka kwa kufanya mikutano mbalimbali na walengwa tofauti kama vile wasimamizi wa mitihani ya kidato cha nne, wafanyabiashara, wadau kutoka jumuiya za kidini na zisizo za kiserikali, watumishi wa umma kwa vile kwa kiwango kikubwa vitendo vya namna hii hutokea katika sekta hizo.

Mheshimiwa Spika; Kamati inaipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Mamlaka hii kwa kuingiza katika shughuli zao elimu ya rushwa na uhujumu wa uchumi katika Tamasha la Elimu Bila Malipo la Zanzibar lililofanyika mwaka *2018*, ambapo mashindano ya ngazi ya taifa ya Kongamano, *"Quiz (general knowledge)"* na Mdahalo. Kwa hakika, shughuli hizo zimetoa ufahamu kwa kiasi kikubwa kwa wanafunzi, wazee, walezi na wananchi waliohudhuria au kufuatilia shughuli hizo. Hivyo, Kamati inasisitiza kuendelea kwa utaratibu huu katika matamasha mengine mbalimbali. Aidha, Kamati inaomba pia kuwe na utaratibu wa kutoa mafunzo kwa njia ya filamu.

Mheshimiwa Spika; sambamba na hayo, Kamati inasisitiza kukamilishwa kwa utaratibu wa kuandaa mada zinazohusiana na rushwa na uhujumu wa uchumi katika mitaala ya elimu ili kuhakikisha kwamba elimu ya rushwa na uhujumu wa uchumi inafundishwa katika ngazi zote za elimu.

Mheshimiwa Spika; vilevile, Kamati imeridhishwa sana na hatua zilizofikiwa katika matayarisho ya kujenga jengo la ofisi la Mamlaka ambalo litaleta faraja kwa wananchi pamoja na uongozi na watendaji wa Mamlaka na pia usalama wao na taarifa zinazopokelewa na Mamlaka. Kamati pia, inaishauri Mamlaka

kuangalia uwezekano wa kuanzisha ofisi zao katika kila wilaya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika; Kamati, inawashauri wananchi ambao hutumia mfumo wa kuwasilisha taarifa wa *"hotline "* kupitia nambari *113*, kuitumia fursa hiyo kwa usahihi kabisa ili lengo la kuanzishwa kwa mfumo huo liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika; Kamati pia, inawaomba wananchi, watumishi na wadau kutoa ushirikiano unaohitajika katika kuhakikisha kuwa taarifa sahihi na ushahidi unapatikana kwani kupatikana kwa taarifa na ushahidi unaojitosheleza ndiko kunakoweza kuwatia hatiani wale wote wanaohusika na makosa hayo.

Mheshimiwa Spika; mwisho kabisa, Kamati inaishauri Wizara ya nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuzifanyia kazi changamoto kuu zifuatazo zinazoikabili Mamlaka hii: ukosefu wa vifaa vya kisasa vya kiuchunguzi, ukosefu wa fedha na uhaba wa wataalamu ili Mamlaka iweze kutekeleza vyema majukumu yake pamoja na kufikia malengo yaliyowekwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika; mwisho kabisa, naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii ya maoni ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika; Naomba Kuwasilisha.

.....

(Machano Othman Said)

Mwenyekiti,

Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum

Baraza la Wawakilishi,

Zanzibar